# SOMO MAALUMU LA KARAMA YA NENO LA MAARIFA KWA WANA SAYUNI – JAN 2021

## Maandiko: 1KOR: 12: 4 – 11

1. **UTANGULIZI**
   Karama ya Neno la Maarifa ni ufunuo ambao Roho Mtakatifu anamwonyesha/ anamfunulia mtu wa Mungu kwa lengo la kumtaarifu/ kumjulisha juu ya ukweli fulani wa Neno la Mungu jinsi **lilivyopotoshwa** au **kuachwa** na waalimu wa uongo na manabii wa uongo.

- **Karama ya Neno la Maarifa ni ya muhimu sana kwa Kanisa kwa sababu mojawapo ya mbinu kabambe anayoitumia ibilisi tangu mwanzo ili kupoteza/ kukengeusha wateule wengi ni mbinu ya upotoshaji wa kweli za Neno la Mungu.** ***Mwanzo 3: 1 – 5; 1Timoth 4: 1 – 3; 1Wafal 13: 11 – 19; Luk 4: 1 – 13.***
- Ufunuo huu wa Roho Mtakatifu (Karama ya Neno la maarifa) unaweza kuwa na lengo la kumwonya mtu wa Mungu, au kumtahadharisha au kumpa maelekezo maalumu kuhusu vita iliyopo kati yake au hila za shetani zilizopangwa dhidi yake kwa kusudi la kumwangamiza.
- **Ni ukweli usiopingika kwamba mipango yote ya ibilisi inayopangwa dhidi ya watu wa Mungu, Mungu anaijua yote; na kama wana wa Mungu watapata nafasi ya utulivu kama alivyokuwa mtumishi wa Mungu Elisha, Mungu angewajulisha mipango yote ya adui na hivyo kuwafanya wajiepushe na majanga mengi na kamwe wasingeangamia hovyohovyo tu.** ***2Wafal 6: 8 – 12***. Kukosa neno la maarifa kumepelekea watu wa Mungu kuangamia hovyohovyo hata katika siku zetu. ***Hosea 4: 6***

2. Yesu Kristo katika mafundisho yake ya hotuba ya mlimani; aliwaambia wanafunzi wake msamiati mgumu sana **"Jihadharini na manabii wa uongo; watu wanaowajia wamevaa mavazi ya**

**kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali.** ***Math 7: 15*** na ***Mark 8: 15.*** Yesu aliwaagiza kisema "Angalieni, **jihadharini na chachu ya mafarisayo na chachu ya Herode;** na ***Mark 13: 5*** Yesu anawaonya wanafunzi wake kwa kuwaambia **"Jihadharini; mtu asiwadanganye"** Pasipo kumwomba Mungu ili atupe karama ya Neno la Maarifa, siyo rahisi kuchukua tahadhari hizi ili kuepuka udanganyifu wa hali ya juu na upotoshaji unaofanywa na ibilisi kwa wateule wa Mungu akiwatumia watu waliokubali kuwa mawakala wake hapa duniani.

**Mfano:**

(a) ***Mdo 5: 1 – 11:*** Pasipo Mtume Petro kuwa na Neno la Maarifa/ kupata ufunuo wa jinsi Anania na Safira mkewe walivyokuwa wamepotosha ukweli na kutaka waonekane mbele za Mitume kuwa ni watu watoaji wa kweli na waombewe Baraka toka kwa Mungu; Ona jinsi ambavyo shetani angekuwa anacheka wakati Petro anapoomba Baraka za Mungu zije kwa watu waongo na mawakala wa ibilisi!!

(b) ***2Wafalme 5: 20 – 27:*** Pasipo Nabii Elisha kuwa na karama ya Neno la Maarifa kufunuliwa jinsi mtumishi wake Gehazi alivyopotosha ukweli na kutaka aonekane kuwa hajaenda popote kumbe tayari ameenda kudai fedha kwa Naamani kupitia jina la Elisha kwamba amemtuma!! Aliumbuliwa palepale!!

(c) ***1Samwel 15: 1 – 21***; Pasipo Nabii Samweli kuwa na karama hii ya Neno la Maarifa na kuonyesha jinsi ambavyo Sauli amepotosha maagizo ya Mungu ili ajitajirishe; Sauli alivyokuwa mbishi asingemweza; **na hata leo ndani ya Kanisa watu walio na Roho na sura ya Sauli ya ubishi katika makosa ambayo wameyatenda ni wengi mno.** Bila karama ya Neno la Maarifa; hawa ndiyo watapewa kipaumbele katika huduma kutokana na lugha zao laini na matokeo yake nguvu za Mungu katikati ya Kanisa zinatoweka na tunabaki na ibada za shoo (maonyesho tu)

***Note:*** Upotoshaji wa kweli za Neno la Mungu kwa sasa unafanyika kisayansi mno. ***Dan 12: 4*** Leo mwanamke anakubali kuzalishwa na mbegu zisizokuwa za mume wake (Artificial incermination) kama ng'ombe wanavyozalishwa; kuna **unene** wa bandia; **uzuri** wa bandia; **miujiza** bandia n.k. Pasipo karama ya Neno la Maarifa siyo rahisi kujua utendaji huu bandia wa shetani.

3. ***Mark 8: 15 –*** Kujilinda na chachu ya mafarisayo na chachu ya Herode ambayo ni unafiki siyo jambo jepesi bila kuwa na Neno la Maarifa. ***Luk 12: 1.*** Neno la Maarifa linahusu kweli za Mungu ambazo tayari zimekwisha potoshwa (past) na ambazo zinapotoshwa mpaka sasa (present) tofauti na karama ya Neno la Hekima kama tulivyoona huko nyuma kwamba yenyewe inahusiana na mipango aliyonayo Mungu wetu kwa ajili ya siku zetu za mbele (usoni) (future)

- Unaonaje kama Yesu asingekuwa na karama ya Neno la Maarifa wakati shetani amemjia **kinafiki** na lugha **laini** kama ya upendo na kumhurumia baada ya kukaa siku 40 pasipo kula chakula!! ***Luk 4: 1 – 13.*** Shetani alitumia **maandiko** ili ampotoshe Yesu kama alivyotumia maandiko na kufanikiwa kumpotosha Hawa na baadae Adamu. Hii ndiyo chachu ya mafarisayo na chachu ya Herode (wakuu wa dini na watawala Serikali) wote wanatumia Neno la Mungu kwa hila ili kupotosha wateule. Hila ilitumika kupotosha ukweli wa ubatizo wa maji mengi kupitia **mfalme Constantine na wakuu wa dini** wakashikilia kwa ajili ya kulinda heshima za dini zao.

- Nasema kweli kabisa, wateule hadi sasa tuko katika vita vikali mno ya kiroho na adui yetu shetani tukipambana na nguvu zake za uongo na hila nyingi zisizoonekana kwa macho haya ya nyama lakini ni nguvu halisi kabisa zinazotenda kazi – ***Efeso 6: 12 – 13.*** Bila karama ya Neno la Maarifa kamwe hatutaweza kumshinda ibilisi na hila zake anazokuja nazo kwetu; yeye yu tayari kuja kwetu kama malaika wa Nuru kwa lugha ya **upole na upendo** na

**ukarimu** lakini lengo lake likiwa lilelile la kutupotosha na kutukengeusha. ***2Kor 11: 13 – 14.***

- Alijigeuza kwa Mitume ili aonekane kama mtoaji halisi kupitia Anania na Safira – akagundulika.
- Alijigeuza kwa Yesu akagundulika.
- Akajigeuza kwa Nabii kijana ili aonekane amejaa huruma na ukarimu akafanikiwa.
  “Yaani njia maalumu na **mbinu** yake ya hali ya juu anayoitumia ili kutukengeusha ni **kutwist** kweli za Neno la Mungu kwanza, na kama hatuna karama ya Neno la Maarifa ili tugundue upotoshaji huu mapema na kuukemea tutajikuta tumebaki na jina tu la kuokoka lakini ni wagomvi wakubwa mioyoni mwetu na kweli za Neno la Mungu wetu zilizoandikwa.

4. Yesu kwa kuwa na karama ya Neno la Maarifa na kwa kujaa Neno la Mungu; alifanikiwa kupinga hoja zote za ibilisi. Na kila mteule leo anakutana na mitihani tofautitofauti ya maisha haya akiwa ndani ya wokovu; pasipo kujaa karama ya Neno la maarifa utajikuta unaunga mkono maneno ya adui na kupotosha kweli ya Neno la Mungu kama walivyofanya wana wa Israeli na wengi wakafa jangwani. ***Kut 14 :10 – 12;*** Lakini kusudi la Mungu la kutuokoa ni ili atujaze na karama ya Neno la maarifa kama alivyofanya kwa Musa ili saa ya majaribu makubwa sisi tuwe na ufunuo unaotuwezesha kutambua kweli za Mungu wetu kwamba ametuokoa na anatupigania daima. ***Kut 14: 13 – 25.***

- Ni wakati muafaka sasa kwa kila mteule kumwomba Mungu karama hii ya Neno la Maarifa maadamu ametambua umuhimu wake katika maisha yake ya kiroho na katika vita yake anayokutana nayo siku kwa siku katika jina la Yesu Kristo – Amen.

**Na**
**Askofu Dr. L. M. Mwizarubi**
**Jan 2021**